JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUHEZA HIGH SCHOOL

MAY, …………………..
Muheza, Tanga

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA MUHEZA

Simu MKUU WA SHULE: +255 652 448 655
E-mail: muhezahighschool@gmail.com
Makamu MKUU WA SHULE 0653517606
Malezi: 0755692575
Kumb Na. MHS/ ADM /JI/2O25/ ………

MUHEZA HIGH SCHOOL
S.L.P 420,
60 MANG'ENYA ROAD
MUHEZA
Tarehe:… … … … … … …

Mzazi/Mlezi wa …….. **………**………………………………kidato cha……**……**……………
**S.L.P ………………**

Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MUHEZA HIGH HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA. MKOA WA TANGA MWAKA WA MASOMO ………………………

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka ……………… na atasoma tahasusi ya …………

   Shule ya sekondari MUHEZA HIGH ipo umbali wa kilometa tatu (3) mashariki mwa mji wa MUHEZA, Usafiri wa taksi kutoka mjini MUHEZA unapatikana kwa nauli ya Shilingi 5,000/=; kwa pikipiki Shilingi 1,500/= na kwa bajaji shilingi 3,000/=

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

   i. Sare ya shule hii kwa wavulana ni mashati 2 light blue (Bluu Bahari) ya mikono mirefu yasiyobana na suruali 2 dark blue zenye mifuko 2 mbele na 1 nyuma isiyo ya kubandika, iwe ndefu hadi kiwiko cha mguu, isipungue upana wa chini inchi 14 chini na mkanda wa suruari mweusi wa ngozi.Kwa wasichana ni mashati 2 light blue (BluuBahari) ya mikono mirefu yasiyobana na sketi 2 dark blue ndefu mpaka karibu na viatu zenye linda box isiyobana; Kwa wanaovaa Hijabu, rangi ya hijabu ifanane na sare ya shule (Hijabu light blue-Bluu Bahari) bila urembo wa aina yoyote ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama na sketi 2 dark blue ndefu mpaka kiwiko cha mguu zenye marinda ya linda box na isiyobana. Pia

fulana ya shule yenye nembo kwa wavulana na wasichana (**Kwa anayehitaji** zinapatika shuleni kwa gharama ya Tsh.15000/=

ii. Shamba dress: wavulana suruali nyeusi (aje nayo) na fulana ya blue yenye nembo ya shule, fulana ya bluu yenye nembo ya shule **kwa anayehitaji** inapatikana shuleni kwa gharama ya Tsh. 15000/=. Wasichana aje na gauni la dark green refu mpaka kwenye kiwiko cha mguu na lisilo na marinda na wanaotumia hijabu (kijuba) ni rangi moja na gauni.

iii. Sare ya shule kwa michezo ni track suit mbili dark blue kwa wavulana na kwa wasichana ni dark green. Na raba za michezo nyeupe kwa wote.
Angalizo:*Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani Zaidi ya zilizotajwa hapo juu.*

iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

v. Soksi jozi mbili nyeupe/nyeusi za shule;

Vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;

vi. Sweta rangi ya darkblue lenye nembo ya shule **kwa anayehitaji** linapatikana shuleni kwa bei ya Tsh.15000/=

NB:kwa atakayepata changamoto ya upatikanaji wa sare za shule awasiliane na uongozi wa shule kwa maelekezo zaidi.

2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari counter book 4 quire tisa (9) na daftari za kawaida za mazoezi angalau moja kwa kila somo;

ii. Ream nne (A4 duplicating papers) za Karatasi kwa mwaka;

iii. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology kwa ajili ya mazoezi ya upasuaji wa chura, Mende,Panya n.k

iv. Scientific Calculator fx991

v. Godoro 1 na foronya yake (futi 3 kwa 6) na Chandarua (Neti) kwa ajili ya kujikinga na Mbu rangi ya blue. Mto na foronya yake rangi ya blue.

vi. Shuka jozi 2 za blue.

vii. Nguo za ndani za kutosha;

viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);

ix. Ndoo 2 ndogo zenye mifuniko (za lita kumi);

x. Aje na Bima ya afya ya NHIF
xi. Vifaa vya usafi: - PCB walete Jembe na mpini wake., Kwanja, fagio la Ndani (soft broom) na la nje la mti na
xii. CBG walete Panga, hard broom, squeezer, long cobweb brush, fagio la mti la nje.
xiii.

**2.3 Michango mbalimbali**

Kwa kuwa mwanao atasoma shule ya Bweni

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

Tunashauri ingiza kwenye akaunti ya shule ya Muheza High school NMB Ac. Na. 41901100027 kwa usalama wa fedha husika. Aje na hati ya malipo (bank pay in slip) halisi yenye jina la mwanafunzi husika ya benki ya NMB aliyolipia michango tajwa hapo juu. *HATUPOKEI FEDHA TASLIMU*.

3:0. Sheria na kanuni za shule hii.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
viii. Kutunza mali za shule;
ix. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
x. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

MUHIMU:

- ❖ Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;
- ❖ Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;
- ❖ Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).
- ❖ Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;

3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

3.3 Fomu muhimu za kujaza mwanafunzi aje nazo shuleni

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai; nakala ya results slip na leaving certificate ya kidato cha nne
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

4 Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA MUHEZA HIGH SCHOOL

……………………………………….
B.H.KINYEMI
MKUU WA SHULE

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI U P A T A P O U J U M B E WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

- Mkuu wa shule: 0652448655
- Makamu Mkuu wa Shule: 0653517606
- Mwandamizi Malezi: 0755692575

FOMU YA KUKIRI KUJIUNGA NA SHULE (Ijazwe na mwanafunzi)

Jina la mwanafunzi------------------------------
S.L.P----------------------------------------------
----------------------------------------------
Tarehe----------------------------------------

MKUU WA SHULE,
MUHEZA HIGH SCHOOL,
S.L.P . 420,
MUHEZA.

YAH; FOMU YA KUKIRI UCHAGUZI WA KUJIUNGA NA KIDATO **CHA TANO ……………………….**

1. Ahsante sana kwa barua yako yenye kumb.MHS/ADM/JI/2023/…………….ya tarehe ………………….ya kunijulisha kuwa nimechaguliwa kujiunga na kidato cha tano shuleni hapo.
2. Ninatoa ahadi kutii sheria zote za shule ambazo nimezisoma na kuzielewa.
3. Ninakubali / sikubali nafasi hii niliyopewa na Taifa.
4. Niko tayari kutimiza maagizo yote niliyopewa ya kujiunga na shule hii.
5. Historia fupi ya mwanafunzi husika.

PICHA YA MWANAFUNZI

| Jina kamili uliloandikishwa shuleni | Shule ya msingi na sekondari ulizopitia | Tarehe ya kuzaliwa | Mahali /Wilaya ulipozaliwa | Dini /Dhehebu lako |
|---|---|---|---|---|
| | MSINGI: | | | |
| | | | | |
| | SEKONDARI: | | | |
| | | | | |

Nakiri kuwa maelekezo yote niliyotoa hapo juu ni sahihi.
6.0 Jina kamili la mwanafunzi……………………………sahihi……………..
terehe………………………

7.0 Sehemu ya mzazi/mlezi kukubali kuchaguliwa kwa mwanafunzi husika.

PICHA YA MZAI/MLEZI

7.1 Jina la mzazi/mlezi:…………………………………Kazi: ……………………
Kata mzazi anapoishi…………………… kijiji / mtaa……wilaya………………

Namba ya simu ya mzazi / mlezi : ………………………S.L.P. …………………
Nakiri kuwa huyu ni mwanangu. Nakubali /Sikubali na fasi hii aliyopewa ya kujiunga na shule hii. Nakubaliana / Sikubaliani na sheria na maagizo yote ya shule aliyopewa ya kujiunga na shule hii. Naahidi kumuhudumia mwanangu kikamilifu na kushirikiana na uongozi wa shule katika kufanikisha maendeleo ya elimu yake.

Sahihi ya mzazi/mlezi…………………………….Tarehe:………/………20……
*FUTA ISIYO HUSIKA*

## SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

TO THE MEDICAL OFFICER

---------------------------------------------------
---------------------------------------------------
---------------------------------------------------

Name of student ---------------------------------------------------------------------------------------
Form ---------------------------- Term --------------------------- Year ----------------------------

Dear Doctor

Please kindly examine the above named student to prove his/her fitness undertaking studies at our school.

1. X-ray ( ) 2. Urine ( ) 3. Stool ( )

4. Physical fitness ( ) 5. V.D ( ) 6. Tuberculosis ( )

**A: (I) PRELIMINARY INFORMATION (BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR)**

| NO | DISEASE | YES/NO | NO | DISEASE | YES/NO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | 10 | Epilepsy | |
| 2 | Pneumonia | | 11 | Ear, Nose and threat | |
| 3 | Asthma | | 12 | Skin disorder disease | |
| 4 | Heart trouble | | 13 | Anemia | |
| 5 | Recurrent indigestion | | 14 | Operations | |
| 6 | Jaundice | | 15 | Serious Accident | |
| 7 | Dysentery | | 16 | Malaria | |
| 8 | Kidney and urinary trouble | | 17 | Stomach trouble | |
| 9 | Nervous breakdown | | 18 | Eye disorder | |

**(II) VACCINATIONS AND INNOVULATIONS HISOTRY**

| DISEASE | 1ST DATE | 2ND DATE | 3RD DATE |
|---|---|---|---|
| Small pox | | | |
| Whooping cough | | | |
| Measles | | | |
| Yellow fever | | | |
| Cholera | | | |

**Official**

**B: MEDICAL EXAMINATION REPORT**

(a) Weight

(b) Heat Beat

(c) Vision etc

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above and consider that he/she is physically fit/unfit to undergo studies.

DOCTOR'S NAME & SIGNATURE ---------------------------------------------------------------------------------

DATE -------------------------------------